# UTANDAWAZI NA DHIMA YA KISWAHILI KAMA LUGHA YA AFRIKA MASHARIKI

P. Mtesigwa

**Ikisiri**

Neno "utandawazi" limevuma na kusambaa kwa kasi kubwa kati ya maneno mapya yaliyoibuka enzi za karibuni katika lugha ya Kiswahili. Kusambaa kwa neno hili ni ushahidi tosha kwamba dhana ya utandawazi inayobebwa na neno hili inagusa nyanja mbalimbali za maisha katika jamii – siasa, uchumi, uandishi wa habari, elimu, utamaduni, sayansi na tekinolojia na nyanja nyingi nyinginezo. Kutokana na kusambaa huko katika matumizi inawezekana neno "utandawazi" likawa na maana zinazotofautiana kidogo kutoka uwanja hadi uwanja. Katika kutazama fasili mbalimbali za neno hilo, makala hii inabainisha kuwa tunaweza kujua ipi ni dhana ya msingi ambayo huzingatiwa hata kama pengine maelezo ya maana ya neno hutofautiana kutoka uwanja hadi uwanja. Makala inaonyesha kuwa nyingi kati ya fasili zilizowahi kutolewa huyagusa maisha ya wanajamii wengi katika jamii mbalimbali hasa katika nyaja za uchumi, siasa na utamaduni kwa jumla ambamo lugha hupata nafasi ya pekee.

## 1.0 Utangulizi

Kwa mujibu wa Little (1996), msingi wa dhana ya utandawazi ni ile fikra kwamba mipango yote ya kiuchumi, kisiasa na hata kiutamaduni inapaswa kuandaliwa kwa lengo la kuondoa mipaka ya taifa moja ili kuiwezesha mipango kama hiyo kutandaa na hatimaye kuitagaa dunia nzima. Kwa msingi huo basi, hatimaye mipaka ya kijiografia haina budi ififie na hivyo kuacha kuwa suala la thamani linalopaswa kuzingatiwa katika mipango au fikra za aina yoyote katika nyanja za maendeleo mbalimbali ya jamii.

Mathalani kwa upande wa uchumi Little (1996) anafafanua kwamba utandawazi ni dhati ya kuondoa vikwazo vyovyote vya kijiografia au kisiasa ili kuruhusu mtiririko huru wa nguvukazi baina ya mataifa, uzalishaji mali kwa gharama ndogo na hivyo kufikia upeo wa faida kwa kuuza katika soko huria. Ufafanuzi huu wa kiuchumi unachukuana sana na ule uliotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF 1997) kwamba "utandawazi ni tukio la ushirikishwaji na uunganishwaji wa masoko ya bidhaa na huduma na hali kadhalika mtaji" (uk. 112. Tafsiri yangu).

Kwa upande wa siasa, Little (1996) anaufafanua utandawazi kama dhana inayolenga katika upunguzaji na hata uondoaji wa mamlaka ya dola katika nchi na kupunguza utitiri wa mifumo ya nguvu za dola hata katika kiwango cha kanda za Kimataifa na hivyo kuzidisha mamlaka ya Mashirika ya Kibiashara ya Kimataifa ili kudhibiti uwezo wa mashirika ya kitaifa; yale yanayotawala biashara ya taifa moja husika. Kwa maelezo rahisi ya dhana hii, uamuzi wa kuendesha taifa hata kisiasa unapaswa ulenge kukidhi maslahi ya siasa za kimataifa. Kwa hali hiyo, thamani ya utaifa hupungua polepole na thamani ya ukimataifa huzidi kuimarishwa na kuongezeka. Vivyo hivyo kadri amali za kisiasa za kitaifa zinavyozidi kupungua ndivyo pia amali za kisiasa za kimataifa zinavyozidi kuimarishwa na kuongezeka.

Kwa upande wa utamaduni, Little (1996) anafafanua kwamba utandawazi ni usambazaji habari, amali na usawiri mpya wa kuitazama dunia inayoenenda kwa utamaduni unaofanana pote duniani. Kwa maneno mengine, kwa kutumia tekinolojia ya kisasa ya kusikia na kuona, mfumo maalumu unaozingatia kutamalaki mataifa yote huimarishwa na kuzidi kuenea bila kujali utamaduni wa jamii au mipaka ya kijiografia ya taifa moja. Na kama ilivyo katika nyanja za uchumi na siasa, lengo ni kudhoofisha utamaduni uliojikita katika mipaka ya jamii au taifa mahsusi na badala yake kuzagaza na kustawisha utamaduni wa kimataifa. Sweeting (1996) kwa maneno machache zaidi anafafanua bayana maana ya utandawazi asemapo:

> Unaihusisha dunia yote, ambayo ndiyo sayari mama na maskani kwetu sisi sote. Ni kuiona *dunia kama kitu kimoja* yaani, *kijiji kimoja* na watu wote waliomo kama *kabila moja* (uk 380 – Tafsiri na mkazo ni vyangu).

Pasipo shaka fasili zilizotolewa zinachochea mtu kujiuliza maswali mengi. Miongoni mwake yakiwa ni: Je "Jumbe" wa "kijiji" hiki ni nani aliye na mamlaka ya kudhoofisha na hata kufutilia mbali mamlaka ya dola au mipaka ya taifa au jamii mahsusi? Je "Jumbe" huyu anatenda haya kwa faida ya nani – kwa faida yake binafsi au kweli kwa maslahi ya kijiji? Vyovyote iwavyo, jambo lililo wazi ni kwamba ili utandawazi uweze kustawi hapana budi "Jumbe" anayeusimamia awe na nguvu kushinda upande wa pili wa "watandawazwa". Katika uhusiano kama huo ambapo upande mmoja kuna "watandawaza" na upande wa pili "watandawazwa" je uhusiano huo sio ule anaouita Chachage (2003) wa baina ya "mbilikimo" na "pandikizi" ambako haiwezekani kuwepo soko huria, siasa huria wala utamaduni huria baina ya pande hizi? Mbilikimo atakuwa na uhuru na nafasi sawa na Pandikizi? Lakini je juu ya yote, hivi si kweli kwamba ili kuishi katika *kijiji cha dunia moja* kama ambavyo dhana ya utandawazi ipasavyo kueleweka bila kupotoka, si dhahiri kwamba kila mwanakijiji anapaswa kuwa na nafasi ya kuchangia maendeleo ya kustawisha kijiji hicho?

Dhati ya makala hii ni kwamba mojawapo ya michango inayopaswa kutolewa na "wanakijiji" katika utandawazi ni lugha. Lugha ni mchango wenye upekee katika utandawazi sio kwa sababu tu ndicho chombo cha mawasiliano kinachowawezesha watu wa jamii moja kuwasiliana kati yao na pia kati yao na watu wa jamii nyingine ila pia ni chombo kinachotambulisha na kubainisha watu wa jamii moja na nyingine katika upekee wao. Pasipo lugha hakuna mawasiliano wala hakuna maelewano. Mafanikio yoyote ya siasa, biashara, elimu, tekinolojia, utawala n.k. pamoja na mfumo wa utandawazi wenyewe, huchukulia kuwepo kwa lugha inayoziunga pande zinazohusika. Katika nchi za Afrika Mashariki lugha ya Kiswahili ina dhima ya pekee baina ya wenyeji wengi waishio katika eneo zima la nchi za Maziwa Makuu na pia katika kushiriki katika utandawazi. Kwa hiyo, kama ilivyokwisha kudokezwa, nchi zitakazozungumziwa hasa ni Kenya, Uganda, Tanzania, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Nchi hizi zinachangia mipaka, zinachangia historia, na zaidi ya yote hayo, zinachangia lugha ya Kiswahili inayozungumzwa katika kila moja ya nchi hizo.

## 2.0 Dhima ya Kiswahili katika Afrika Mashariki

## 2.1 Hadhi na Matumizi

Mojawapo ya sababu kubwa ambazo zimedumisha kuwepo uhusiano mahsusi kati ya Nchi za Maziwa Makuu mbali na kuwa majirani, ni lugha ya Kiswahili. Telmans (1978) aliwahi kukadiria kwamba hadi mwaka 1978 kulikuwa na wazungumzaji wa Kiswahili wapatao 47,286,000 aliokuwa amechambua idadi yao kadri ya kila nchi wanamokaa kama ifutavyo:

| | |
|---|---|
| Burundi | 2,650,00 |
| Kenya | 9,104,00 |
| Rwanda | 2,850,000 |
| Tanzania | 10,310,000 |
| Uganda | 7,367,000 |
| Zaire | 15,000,000 |
| Jumla | **47,286,00** |

Kwa mujibu wa Hinnrebusch na Mirza (1979) watu kati ya milioni 60 na 80 wanazungumza Kiswahili hasa ikizingatiwa kwamba idadi ya wazungumzaji wa Kiswahili nchini Tanzania pasipo shaka ilikuwa kubwa kuliko makadirio ya Telmans. Hivi leo inakadiriwa kwamba watu kati ya millioni 80 na 100 huzungumza Kiswahili katika nchi hizi kwa viwango mbalimbali. Katika Afrika Mashariki (Kenya, Tanzania na Uganda) peke yake inakadiriwa kwamba watu kiasi cha millioni 50 huzungumza Kiswahili. Kadhalika inakisiwa kwamba theluthi mbili za wakazi wote wa Afrika Mashariki wanaweza kuzungumza Kiswahili kwa kiwango cha kueleweka.

Kwa upande wa hadhi, Kiswahili kina hadhi ya viwango mbalimbali vya matumizi katika nchi mbalimbali kinamozungumzwa. Katika Kenya na Tanzania Kiswahili ni lugha ya taifa na pia mojawapo ya lugha rasmi. Katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambako Kiswahili huzungumzwa hasa sehemu za Mashariki za nchi hiyo, Jimbo la Shaba na pia katika miji mikubwa yote ya nchi hiyo, Kiswahili ni mojawapo ya lugha nne za taifa (lugha zingine ni Kilingala, Kikongo na Chiluba). Uhusiano wa biashara na mwingiliano wa kisiasa ulioongezeka, na unaozidi kuongezeka, katika miaka ya karibuni baina ya Kongo na Tanzania umezidi kueneza pia matumizi ya Kiswahili nchini Kongo.

Katika nchi za Uganda, Rwanda, na Burundi Kiswahili kinatumika kama lugha ya mawasiliano mapana. Katika nchi hizi watu wawili wasiozungumza lugha ileile ya kikabila wakutanapo, upo uwezekano mkubwa kwamba watazungumza Kiswahili kama hawatazungumza ama Kiingereza au Kifaransa. Kiswahili hutumika katika majeshi takriban katika nchi zote za Maziwa Makuu. Katika vyombo vya habari, hasa katika idhaa za radio na televisheni, Kiswahili ni lugha maarufu na muhimu karibu katika kila mojawapo ya nchi hizo. Mbali ya kuendelea kuwa lugha ya kukuza biashara kati ya mataifa hayo Kiswahili kinazidi kuwa lugha ya kujenga udugu baina ya wakazi wa Nchi za Maziwa Makuu katika kutafuta suluhisho la matatizo yao ya vita vya wenyewe kwa wenyewe. Pasipo shaka ingawa mikataba ya makubaliano huandikwa kwa lugha za kigeni lakini pale mazungumzo ya kidugu yanapopewa nafasi ya kufanyika, Kiswahili hupata nafasi ya kutumika. Kama Kiswahili ndiyo lugha inayotumika katika mafunzo na shughuli nyingine za askari kambini, bila shaka ndiyo lugha itakayowezesha mapatano baina ya askari haohao wasipigane pia.

## 2.2 Historia na mweneo wa Kiswahili kwa muhtasari

Kwa mujibu wa Mazrui na Mazrui (1995) Kiswahili ni lugha ya Pwani ya Afrika Mashariki na pia ni lugha ya Kibantu ambayo kwa karne nyingi imekuwa na mwingiliano mkubwa na lugha nyingi za kigeni. Kutokana na hali hiyo nguvu za kuenea kwake zimetokana hasa na mambo makuu matatu: biashara, dini na utawala. Kwa upande wa biashara Mazrui na Mazrui (1995) wanaeleza kwamba hata kabla ya karne ya kwanza Kabla ya Kristo (KK), Pwani ya Afrika Mashariki iliwahi kupokea wageni waliofika kutoka nchi za Mashariki ya Kati hasa kutoka Oman, Saudi Arabia, Yemen, Muskat na Ghuba ya Uajemi (Persian Gulf). Waaidha upwa wa Afrika Mashariki ulipata kupokea wageni kutoka Misri na Uyunani. Kadhalika, kwa mujibu wa Whiteley (1969), walikuweko wageni waliowahi kufika Pwani ya Afrika Mashariki kutoka Mashariki ya mbali pia kama vile kutoka Malaysia, Uchina, Hong Kong na hata Japan. Ingawa baadhi ya wageni hawa wa mwanzo waliotajwa hawakuacha athari kubwa kwa upwa huu, lakini walifanya biashara ndogondogo na watu wa Pwani. Baadhi waliacha kumbukumbu za maandishi kama zile za kitabu cha *Periplus of the Erythrean Sea* ambacho inasemekana kiliandikwa na baharia mmoja wa kale mnamo karne ya 1 Baada ya Kristo (BK)

Kuanzia nusu ya pili ya Karne ya Kwanza BK, ndipo uhusiano kati ya Pwani ya Afrika Mashariki na wageni kutoka Mashariki ya Kati ulipokomaa. Wageni waliokuja Pwani ya Afrika Mashariki walianzisha bandari-miji na kukaa kwa ajili ya kufanya biashara pwani. Kati ya miji maarufu kama hiyo iliyoanzishwa na Waarabu ilikuwa Pate, Lamu, Kismayu, Kilwa na Sofala. Kadiri biashara ilivyozidi kushamiri na hasa baada ya biashara ya pembe na watumwa kutoka bara kushika kani ndivyo pia miji mingi ilivyoongezeka Pwani ya Afrika Mashariki na mingine ikaanzishwa kule bara ambayo mwanzo ilikuwa kama vituo maalum vya misafara. Kadiri miaka ilivyopita ndivyo pia biashara hii ilivyopenya mpaka Maziwa Makuu (Z. Nyasa, Z. Tanganyika na Z. Nyanza/Victoria) na hata kuvuka na kuingia nchi za Uganda, Rwanda, Burundi, Kongo, Malawi, Zambia na Msumbiji.

Kwa upande wa lugha ya Kiswahili, lugha hii ilipanuka hasa kutokana na mwingiliano na Kiarabu katika upwa wa Pwani. Hata jina la lugha hii (Kiswahili) lilitokana na neno la Kiarabu "suahel" lenye maana ya "pwani". Kutokana na neno hilo maana halisi ya "Kiswahili" ni "lugha ya Pwani." Hivi leo inakadiriwa kwamba maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu hufikia kati ya asilimia 30 na asilimia 40 (Mazrui na Mazrui 1995, Polome', 1967). Lakini ukweli huu una mambo muhimu mawili ya kuzingatia. Kwanza ni ule ukweli kwamba kabla ya wageni kuwasili pwani kulikuwa na watu walioishi hapo ambao wageni walipofika walifanya biashara nao. Pili, watu hao walikuwa na lugha ambayo Waarabu waliita kwa fasili ya lugha ya Kiarabu "lugha ya pwani" Na hivyo kiwango cha msamiati wenye asili ya Kiarabu haukukigeuza Kiswahili kuwa lugha kizalia (kipijini) au Kiarabu. Muundo wa Kiswahili umebaki uleule kama ulivyo muundo wa lugha za Kibantu katika muundo wa maumbo ya maneno na pia katika miundo ya tungo za lugha hizo. Zaidi ya hayo Kiswahili pia kina asilimia kubwa ya maneno yenye asili ya lugha za Kibantu. Hiki ndicho kigezo sahihi kinachopaswa kutumika katika kukianishia Kiswahili.

Kukua na kuenea kwa Kiswahili kulisaidiwa sana na misafara ya biashara kutoka pwani iliyoingia bara kama ilivyokwishatajwa. Kadiri misafara hii ilivyozidi kupenya bara ndivyo pia lugha ya Kiswahili ilivyozidi kujipenyeza na kuenea bara. Matumizi haya hayakuimarika kutokana na biashara tu bali pia kutokana na matumizi ya Kiswahili katika mafundisho ya dini ya Kiislamu. Wareno walipofika Pwani ya Afrika Mashariki mnamo karne ya 15 walikuta Kiswahii kimekwishashamiri pwani. Katika karne mbili walizokuwa wakitembelea Pwani ya Afrika Mashariki kama kituo cha kuchukulia maji na vyakula katika safari zao za Bara Hindi pamoja na kukusanya kodi hasa katika miji ya Sofala, Kilwa na Mombasa, Wareno hawakujishughulisha sana kupenya bara. Kwa hivyo mbali na maneno machache ya Kireno yaliyojipenyeza katika Kiswahili na kuiga baadhi ya michezo na mavazi yao, Wareno hawakuacha athari kubwa sana Pwani. Leo hii yanaonekana tu magofu na makasiri ya majengo yao lakini kishindo cha kuweko kwao pwani kwa karne mbili si kikubwa sana.

Wamisionari kutoka nchi mbalimbali za Ulaya waliofika Pwani ya Afrika Mashariki katika sehemu ya pili ya karne ya 19 ili kuhubiri dini ya Kikristo walifikia miji ileile ya Waarabu, hasa Mombasa na Zanzibar. Huko walijifunza Kiswahili na walipopenya kuingia bara walipitia njia zilezile zilizokuwa zimetumiwa na misafara ya Waarabu. Mbali na kuhubiri Injili walifungua shule katika vituo vyao. Mashirika mengi yalitumia Kiswahili kuhubiri Injili. Baadhi ya mashirika walitumia lugha za makabila ya huko walikokaa kwa sababu mbili. Kwanza waliamini kwamba kwa kuwa Kiswahili haikuwa lugha ya kwanza ya waumini wao Injili isingewapa mguso uleule kama ambavyo ingehubiriwa katika lugha zao za kienyeji. Pili baadhi ya madhehebu yalihusisha Kiswahili na Uislamu na hivyo kutumia Kiswahili kungepotosha dhana za Kikristo. Matokeo ya mtazamo huo hadi leo yanajidhihirisha kama sababu ya Kiswahili kutopokewa kwa urahisi katika baadhi ya sehemu za nchi za Maziwa Makuu.

Ukoloni uliposhika hatamu katika nchi za Maziwa Makuu mwishoni mwa karne ya 19, kulikuwa na mabadiliko katika matumizi na hata kuenea kwa Kiswahili. Mwanzo nchi za Tanganyika, Rwanda na Burundi zilikuwa koloni moja chini ya himaya ya Mjerumani. Katika hali hiyo Kiswahili kilipata nafasi ya kutumika kama lugha ya mawasiliano katika ngazi ya utawala wa wenyeji na mafunzo ya elimu ya ufundi na ukalimani. Kenya na Uganda yalikuwa makoloni ya Mwingereza japo kwa hadhi tofauti (Kenya ilikuwa koloni kamili ambapo Uganda ilikuwa himaya hifadhiwa). Nchini Uganda Kiswahili kilipambana na lugha ya Luganda ambayo ilitumika kwa mapana na marefu katika matumizi ya kila siku ya ufalme wa Buganda. Nchi ya Kongo ilikuwa koloni la Wabelgiji. Kwa mujibu wa Spencer (1974) sera za wakoloni kuhusu lugha za Kiafrika zilitofautiana. Katika makoloni ya Mmjerumani lugha ya Kiswahili iliachiwa kutumika katika utawala wa ngazi ya wenyeji. Katika makoloni ya Mwingereza lugha za wenyeji ziliachiwa zitumike ili kwa kufanya hivyo wenyeji waendelee kugawanyika na hivyo kurahisisha kazi ya kuwatawala. Katika makoloni ya Wabelgiji, kama yalivyokuwa makoloni ya Wafaransa, lugha za Waafrika hazikutambuliwa kwa hiyo hazikupewa nafasi kabisa. Lengo la Wafaransa lilikuwa ni kuwastaarabisha watu weusi kwa kutumia lugha ya Kifaransa na utamaduni wake. Sera ya Mjerumani, kwa mujibu wa Nurse na

Spear (1985), Kiswahili kiliruhusiwa kutumika katika_ngazi ya utawala wa kienyeji ili wenyeji wasichafue lugha ya mtawala – Kijerumani.

Baada ya Vita Vya Kwanza vya Dunia, Mjerumani alipoteza makoloni yake. Tanganyika ilishikwa na Mwingereza kama mdhamini wa nchi hiyo kwa niaba ya Baraza la Udhamini la Umoja wa Mataifa. Rwanda na Burundi yalikuwa makoloni ya Mbelgiji. Nchi hizi ambazo zilikuwa chini ya himaya ya mkoloni mmoja sasa ziliwekwa chini ya wakoloni tofauti na mbalimbali – "komba wapya msitu mpya!" Mabadiliko haya yaliunda mpangilio mpya hata kwa sera za lugha za kikoloni. Kenya, Uganda na Tanganyika sasa ziliunda kanda iliyoitwa Afrika Mashariki na zikawekwa chini ya sera za lugha za ukoloni wa Mwingereza ambazo ziliruhusu ukuaji wa lugha za kienyeji alimradi hazikuwa na nguvu ya kushindana na Kiingereza. Kwa mtazamo huo ndivyo Kiswahili kilivyokuzwa katika nchi hizo tatu kwa kuteua lahaja moja tu ya Kiunguja kuwa Kiswahili mwaka 1928 na kukiundia Kamati mahsusi ya kusimamia ufasaha na ukuaji wake mwaka 1930 kwa nchi zote tatu. Kwa mujibu wa Whiteley (1969) uteuzi wa Kiunguja kama Kiswahili sanifu ulipata upinzani mkali kutoka kwa watumiaji wa Lahaja ya Kimvita, Kenya. Lahaja ya Kimvita kwa karne nyingi ilikuwa imejenga hazina kubwa ya Kiswahili kwa upande wa fasihi, hasa ushairi. Hatuhitaji kusema mambo mengi hapa kuhusu Kiswahili katika enzi baada ya Vita Kuu ya Kwanza. Jambo moja lililo dhahiri ni kwamba sasa Kiswahili kilipewa msingi mzuri wa kuweza kukomaa kama lugha katika Afrika Mashariki nzima.

Kwa upande wa Rwanda na Burundi baada ya kutwaliwa na Mbelgiji nchi hizo hazikuhesabiwa tena kama sehemu ya eneo la kanda moja na Tanganyika kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni wa Mjerumani. Badala yake ziliunganishwa na Kongo na kuhesabiwa kama sehemu ya Afrika ya kati chini ya sera za lugha za ukoloni wa Kibelgiji. Kuendelea kutumika kwa Kirundi na Kinyarwanda ambazo kwa hakika ni lugha zinazokaribiana sana kumetokana na ukweli kwamba wazungumzaji wenyeji wa lugha hizo waliendelea kuzitumia katika maisha yao ya kila siku kwa urahisi zaidi pengine kuliko hata Kiswahili, hata kama hazikupewa hadhi yoyote katika macho ya utawala mpya wa ukoloni wa Wabelgiji. Jambo linaloweza kusemwa Kuhusu Kiswahili katika nchi hizo ni kwamba kwa kuwa watu wa nchi za Rwanda na Burundi waliendelea kuwasiliana na kuingiliana na watu wa nchi za Afrika Mashariki, hasa Tanganyika, ambako Kiswahili kilikuwa kimepewa fursa ya kukua na kuimarika, basi haikuwa rahisi kukiua moja kwa moja katika nchi za Rwanda na Burundi. Kadhalika cheche zilizokuwa zimekieneza huko tangu enzi za biashara ya Waarabu na pia_ukoloni wa Mjerumani hazikuwa rahisi kuzimwa. Hivi ndivyo tunavyoweza kusema pia kuhusu Kiswahili nchini Kongo hasa sehemu za Mashariki na Kusini Mashariki kwa kuzingatia jinsi lugha hii ilivyopata kufika enzi za misafara ya Waarabu kutoka pwani.

**2.3 Harakati za Uhuru na matokeo yake**

Vuguvugu la kujitawala lilipoanza kuumuka katika bara la Afrika, nchi za Maziwa Makuu hazikubaki nyuma. Ngao kubwa katika harakati za kutafuta uhuru ilikuwa ni kuunda umoja wa kitaifa katika kila nchi husika na lugha ya kuwaunganisha watu ilikuwa

kipengele muhimu katika kuunda umoja huo. Ndipo hali halisi ilipojidhihirisha, hasa kuhusu nafasi ya Kiswahili au lugha nyingine za wenyeji wa nchi zile.

Kwa upande wa Tanganyika, Kiswahili kilikuwa kimeenea karibu kila kona ya nchi, hivyo haikuwa vigumu kukitumia katika harakati za kutafuta uhuru. Ilikuwa ni lugha iliyoweza kuwaunga kwa urahisi viongozi, wanasiasa na umma. Katika nchi zingine za Afrika Mashariki hali haikuwa rahisi kiasi hicho. Nchini Kenya na Uganda Kiswahili hakikuwa kimeenea na kusambaa miongoni mwa wananchi wengi kama Tanganyika. Kwa hiyo mawasiliano baina ya viongozi wa siasa na umma yalifanyika ama kwa kutumia lugha za kikabila (kutegemea mahali) au kwa lugha ya Kiingereza. Katika nchi za Kongo, Rwanda na Burundi mawasiliano baina ya viongozi wa siasa na umma yalifanyika katika lugha za_Kirundi (Burundi) na Kinyarwanda (Rwanda) na pia Kifaransa. Kwa upande wa Kongo mawasiliano yalifanyika katika lugha ya Kifaransa lakini katika maeneo yaliyokuwa na lugha kuu moja ya kienyeji yalifanyika kwa lugha hiyo. Ndivyo Kiswahili kilivyopata nafasi ya kuendelea kutumika katika sehemu za Mashariki na Kusini Mashariki katika Jimbo la Katanga (Jimbo la Shaba kwa siku hizi).

Baada ya uhuru suala la lugha liliendelezwa; maana mbali na kuendelea kuwa chombo cha mawasiliano, lugha ilibidi sasa idumishe umoja wa kitaifa uliokuwa umejengwa wakati wa harakati za kutafuta uhuru. Lakini, kama asemavyo Bamgbose (1991) lugha za Kiafrika zilizokuwa zimefanya kazi ya kuleta uhuru ilibidi zifanye kazi ya kuimarisha umoja na zaidi ya hayo kudumisha utambulisho wa nchi. Suala la utambulisho limekuwa zito hasa katika Bara la Afrika ambako takriban kila nchi ina lugha zaidi ya moja. Kwa hiyo suala la kuteua Lugha ya taifa limekuwa nyeti wakati wote; maana lugha kama hiyo inapaswa pia iwe kitambulisho cha taifa linalohusika ambacho pia hulipambanua taifa hilo na mataifa mengine. Kwa upande wa Tanganyika haikua vigumu kukitangaza Kiswahili kuwa lugha ya taifa. Historia ya Kiswahili, kuenea kwake tangu enzi za misafara ya biashara ya Mwarabu pamoja na raghba ya kukitumia katika harakati za kutafuta Uhuru, yote haya yalikuwa yamejenga msingi imara katika nchi hiyo. Vilevile kutangaza Kirundi kuwa lugha ya taifa nchini Burundi au Kinyarwanda nchini Rwanda hapakuwa na tatizo kubwa. Lugha hizo kwa hakika ndivyo vitambulisho vya dhahiri katika mataifa hayo. Katika nchi zilizo na lugha zingine za kikabila zenye nguvu, kutambua Kiswahili kama lugha ya taifa wakati mwingine kumezua sababu ya kukikataa Kiswahili kwa kukihusisha na matukio hasi ya kihistoria kama vile Kiswahili kuwa lugha inayofaa kwa biashara tu, lugha ya wafanya biashara laghai, lugha ya watumwa, lugha ya Waislamu, lugha ya Wajamaa n.k. Katika nchi za Afrika Mashariki hisi hii hasi imewahi kusemwa kwa kejeli kuwa Kiswahili kilizaliwa Tanzania, kikakulia Kenya na kuzikwa Uganda. Hii ishara tosha ya kuwepo matatizo yanayopaswa yazungumziwe na kupatiwa ufumbuzi mbali na kwamba Kiswahili kimeenea sehenu nyingi na kina umuhimu wa pekee kwa wenyeji wa Afrika Mashariki na nchi za Maziwa Makuu.

## 3.0 Matatizo ya Kuimarisha Kiswahili katika nchi za Maziwa Makuu

Katika enzi hizi za utandawazi, Kiswahili kinakumbana na matatizo mengi juu ya yale yaliyokwishagusiwa katika makala haya. Baadhi yake ni haya yafuatayo:

3.1 Hakuna chombo madhubuti kinachosimama ukuzaji, matumizi na uenezaji wa Kiswahili katika kanda yote ya Maziwa Makuu. Mathalani hata katika Katiba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (2002: kifungu 137) imeelezwa kwamba Kiingereza ndiyo itakayokuwa lugha rasmi ya Jumuiiya na Kiswahili kitakuzwa kama lugha ya mawasiliano mapana (lingua fanca). Hali hii inasabibisha misigano hata katika mambo ya msingi kama vile istilahi na vigezo vya ufasaha na Kiswahili na hata mbinu za kukifundisha kama lugha na pia kama taaluma. Kadhalika hali hii inaviza msukumo wa kukazania utumiaji wa Kiswahili katika ngazi mbalimbali ndani ya Afrika Mashariki kwenyewe. Hofu kwamba Kiswahili kitawatenga watumiaji wake na ulimwengu wa maendeleo ya tekinolojia ya kisasa ambayo yanaendeshwa na lugha za Kimataifa, hasa Kiingereza inazidi kupandikizwa. Hofu hii imetawala, na inazidi kuimarika, hata katika nchi ambazo hazina sababu imara za kukataa Kiswahili. Kiingereza sasa ni kigezo cha kupata elimu na ajira.

3.2 Mikakati na hatua za makusudi zinazofanywa na mashirika ya Kimataifa kama Benki ya Dunia na Shirika la fedha la Kimataifa kutotoa huduma zake iwapo Kiswahili kitatumika. Nchini Tanzania, mathalani, shirika la Misaada la Uingereza lilitoa msaada wa kufufua ukuzaji na uimarishaji wa Kiingereza nchini kwa masharti kwamba lazima kiendelee kutumika kama lugha ya kufundishia katika Elimu ya Juu. Nchini Uganda baadhi ya Mashirika ya Misaada kutoka nje yametishia kusitisha misaada yao iwapo Uganda itaamua kufundisha Kiswahili.

3.3 Dhana potofu ya kwamba utandawazi maana yake ni kukubali kumezwa tu na wala si kuchangia katika maendeleo ya "kijiji kimoja" cha dunia inaelekea kupata utetezi. Jambo linalosahauliwa ni kwamba hali hii inasababisha na kuendeleza utegemezi kama nguzo pekee ya kutatua matatizo ya nchi masikini. Utegemezi huu unapewa nguvu si katika masuala ya uchumi tu bali pia katika nyanja zingine za maisha kama ilivyoelezwa katika ufafanuzi wa maana ya utatandawazi.

Yako matatizo makubwa zaidi ya haya yaliyotajwa hapa lakini matatizo haya yanaweza kupewa utatuzi iwapo watu wa Nchi za Maziwa Makuu watakusidia kwa dhati kutatua suala la kutumia Kiswahili kama lugha yao inayowaunganisha. Mathalani, Kwa kuwa sasa Afrika Mashariki tunao umoja wa kiuchumi tunapaswa kujiuliza kama hatupaswi kutoa mchango wetu kwa dunia kwa kutumia lugha ya Kiswahili ambayo inavuka mipaka ya ukabila na hata utaifa kwa faida ya wakazi wote wa nchi hizi na nchi za Maziwa Makuu kwa jumla. Jitihada zilizofanywa na Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki kuunda chama cha ufundishaji wa somo la Kiswahili katika nchi hizi (CHAKAMA), uundaji wa mabaraza ya Kiswahili katika nchi za Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo zilizofanywa hivi karibuni pamoja na bidii zinazofanyawa na vyama vya

Kiswahili nchini Kenya (CHAKITA) na Uganda ni juhudi zinazoleta matumani kwamba utandawazi unapaswa kuwa fursa nyingine inayokipa nafasi Kiswahili kukua na kupanuka kwa upesi na kwa uhakika zaidi.

## 4.0 Hitimisho

Makala hii imeeleza fasili mbalimbali za utandawazi na jinsi dhati yake isivyo kuendeleza usawa baina ya mataifa yenye uwezo na yasiyo na uwezo. Kadhalika imeeleza historia fupi ya chanzo, kuenea na kupanuka kwa matumizi ya Kiswahili katika nchi za Maziwa Makuu ambazo kihistoria zimekuwa na uhusiano wa karibu kama majirani mighairi ya kutengwa na_ukoloni katika enzi mbalimbali. Jambo lililosisitizwa ni kwamba Kiswahili kimekuwa kikiendelea kutumika kwa mawasiliano baina ya wenyeji wa nchi hizi na kutokana na kuenea kwake na kuvunja mipaka ya kikabila na kitaifa, ni lugha yenye sifa ya kuweza kukuza umoja katika nchi hizi. Ushahidi dhahiri wa nguvu hii ni kwamba pamoja na matatizo yote imekuwa vigumu kufutika katika eneo la nchi za Maziwa Makuu. Makala pia imetaja baadhi ya matatizo yaliyopo kuhusu kuimarisha Kiswahili katika nchi za Maziwa Makuu. Baadhi ya matatizo hayo yanatokana na watu wa nchi hizo wenyewe kuogopa kupoteza utambulisho wa lugha au makabila yao na baadhi ni yale yanayotakana na vikwazo vya makusudi vinavyojikita katika dhana potovu ya utandawazi zinazolenga kuimarisha utegemezi. Rai ya makala hii ni kwamba umoja baina ya nchi za Maziwa Makuu ambao umekuwepo kwa karne nyingi za kihistoria unapaswa kuendelezwa zaidi sasa kwa kuimarisha Kiswahili. Tunayo Jumuiya ya kiuchumi ya Nchi za Afrika Mashariki sasa na katika eneo zima tunakabiliana na suala la kutatua migogoro ya kudumisha amani katika nchi hizi. Ili kuwapa nafasi watu wa nchi hizi kushiriki katika utatuzi wa matatizo haya tunapaswa kukipa Kiswahili nafasi ya kutumiwa zaidi. Zipo jitihada zilizofanywa kufikia lengo hilo kwa wapenzi na wasomi wa lugha ya Kiswahili. Hatua muhimu inayotakiwa ni uamuzi na mipango thabiti ya utekelezaji wa serikali za nchi zetu kutathmini, kutumia, kukuza na kuimarisha Kiswahili katika Kanda hii ya Afrika.

## MAREJEO

Bamgbose, A. (1991). *Language and Nation: The National Language Question in Sub Saharan Africa*. Edinburgh: Edinburg University Press.

Chachage, S.L.C. (2003) Kiswahili Katika Muktadha wa Utandawazi (haijachapishwa). Makala yaliyotolewa katika Kongomano la Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili; BAKITA, Dar es Salaam, tarehe 6-7 Febrauri, 2003.

East African Community (2002). *The Treaty for Establishment of the East African Community.* Arusha: EAC Secretarial

International Monetary Fund (IMF) (1997) *World Economic Outlook*. IMF

Little, A.W. (1996) Globalization and Educational Research: Whose Context Counts? *International Journal of Development* Vol. 16, No. 4, uk. 427-438.

Massamba, D.P.B. (2002). Historia ya Kiswahili: 50 BK hadi 1500 BK. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation

Nurse, D. na Spear, T. (1985). *The Swahili: Reconstructing the History and Language of an African Society, 800-1500.*

Mazrui, A. na Mazrui, A.M. (1995) *Swahili State and Society: The Political Economy of an African Language.* Nairobi: East African Educational Pulbishers.

Mdee, J.S. na Mwansoko, H.J.M. (Wah) (2001) *Makala ya Kongamano ya Kimataifa: Kiswahili 2000 Proceedings.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Mlacha, S.A.K. (Mhar.) (1995). *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Phillipson, R. (1992) *Linguistic Imperialism*. Oxford: Oxford University Press.

Polome', E.C. (1967) *Swahili Language Handbook*. Washington DC: Center for Applied Linguistics.

Spencer, J.W. (1974). Colonial Language Policies and their legacies in Sub-Saharan Africa. Katika J.A. Fishman (Mhar.) *Advances in Languages Planning* (uk. 163-175) The Hague:Mouton & Co.

Sweeting, A. (1996). The Globalization of Learning: Paradigm or Paradox? *International Journal of Development* Vol. 16, No. 4, Mk. 379-391.

Telmans, G. M. (1978). *A Morphological Sector Analysis of the Swahili Verb with Implication for the Teaching of English to Speakers of Swahili* Ph.D Dissertation, Columbia University Microfilms. Michigan: Ann Arbor

Whiteley, W.H. (1969*) Swahili: The Rise of a National Language.* London Methuen & Co. Ltd.